# Kilongo cha Unyanyasaji wa Kiusemi katika Mahusiano ya Vijana katika Tamthilia ya *Hatia*: Mkabala wa Uchanganuzi Tunduizi Kilongo wa Kifeministi

Boaz Mutungi
Chuo Kikuu cha Makerere

**Ikisiri**

Makala hii imetumia tamthilia ya *Hatia* katika kufafanua kilongo cha unyanyasaji wa kiusemi baina ya vijana wanaokuwa katika mahusiano ya kutongozana. Unyanyasaji huu unawaathiri vijana wengi. Suala hili linafaa kuchunguzwa kwa sababu vijana wanyanyasaji wanasemekana kuendeleza tabia hiyo hata baadaye katika ndoa zao. Ukilinganishwa na aina nyingine za unyanyasaji katika mahusiano, unyanyasaji wa kiusemi unajitokeza zaidi katika jamii, na madhara yake ni hatari zaidi. Aidha, fasihi inaiga mambo yanayotokea katika jamii huku ikilenga kuboresha jamii hiyo. Vilevile, lugha ya tamthilia inalingana na ya mazungumzo ya kawaida kwa sababu zote zinarejelea mitagusano ya kijamii ambapo wahusika hujibizana moja kwa moja. Kwa kutumia Nadharia ya Uchanganuzi Tunduizi Kilongo wa Kifeministi, makala inadhihirisha kwamba mbali na mamlaka au nguvu za kijinsia, kilongo cha unyanyasaji wa kiusemi kinajikita katika madaraka ya kiumri na ushupavu maalumu wa mhusika au kundi mahususi. Misingi hiyo ya kimamlaka imemwezesha kijana wa kiume kumpuuza, kumkanganya, na hivyo kumdhibiti kwa urahisi kijana wa kike.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii imechukulia mahusiano ya vijana kama mahusiano ya kutongozana. Mahusiano hayo ni ya kimapenzi baina ya binadamu wa kike na wa kiume ambao hawajaoana rasmi. Unyanyasaji baina ya vijana wanaotongozana ni tabia ambapo kijana anamnyanyasa na kumdhibiti mwenzake katika mahusiano ya kutongozana (PCADV, 2011; Apsler & Duggan, 2012). Vijana hawa wanatarajiwa kuwa wamebalehe ambapo, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, wanakuwa na umri wa miaka 15 hadi 24 (WHO, 1989). Kulingana na Wubs na wenzake (2009), unyanyasaji huu ni suala kubwa linalowaathiri vijana wengi kote duniani na unahatarisha afya ya umma (taz. pia Swart na wenzake, 2002). Madhara ya unyanyasaji huu ni pamoja na kuimarisha unyanyasaji katika maisha ya baadaye ya vijana husika (PCADV, *keshatajwa*). Kwa namna hii, unyanyasaji baina ya vijana wanaotongozana unahatarisha asasi muhimu ya ndoa. Vilevile, vijana wengi wanaudhika sana na pengine wanajinyonga (Leaver, 2007; Apsler & Duggan,

*keshatajwa*). Vijana wengine wanaachishwa masomo au kutoroka shuleni (Hagan & Foster, 2001) huku baadhi ya wasichana wakipata mimba za utotoni (Wood & Jewkes, 2001). Kulingana na Wubs na wenzake (*weshatajwa*), wavulana wanashiriki zaidi katika vitendo vya unyanyasaji kuliko wasichana. Hata hivyo, baadhi ya wasichana wanashiriki katika unyanyasaji huu kama njia ya kujitetea dhidi ya unyanyasaji wa wavulana (Lewis & Fremouw, 2001).

Kwa mujibu wa Rubio-Garay na wenzake (2017), unyanyasaji baina ya vijana wanaotongozana unajitokeza kwa njia tatu pana: Kimwili kama vile kupigwa, kung'atwa, na kuchomwa moto; kiusemi kama vile matusi, lawama, vitisho, na kuaibishwa; na kingono kama vile kubakwa. Hata hivyo, makala hii imejikita katika unyanyasaji wa kiusemi kwa sababu mbalimbali. Kwanza, unyanyasaji wa kiusemi unajitokeza zaidi kuliko aina nyingine (Oliveira na wenzake, 2016). Pili, mara nyingi unachochea aina nyingine za unyanyasaji (Salari & Balwin, 2002). Tatu, madhara yake yanadumu milele akilini mwa mnyanyaswaji (Evans, 2006).

Kuna uhusiano mkubwa kati ya unyanyasaji unaopatikana katika jamii na ule unaowasilishwa katika fasihi. Hii ni kwa sababu fasihi inaiga maisha na mahusiano yanayojitokeza katika jamii (Mulokozi, 2017). Aidha, lugha ya tamthilia inalingana sana na ya mazungumzo ya kawaida (Lethbridge & Mildorf, 2004) hasa kwa kuwa yote ni mitagusano ya kijamii ambapo wahusika hujibizana moja kwa moja.

Kwa hivyo, unyanyasaji wa kiusemi katika mahusiano ya vijana ambao unajitokeza katika jamii, pamoja na ule unaosawiriwa katika fasihi, unatumia lugha katika kumuumiza msemeshwaji. Lengo la makala hii ni kufafanua jinsi lugha inavyotimiza kitendo cha unyanyasaji kwa kurejelea tamthilia ya *Hatia* (Muhando, 1972). Tunaangalia jinsi lugha au maneno ya mhusika mmoja yanavyoweza kumnyanyasa mhusika mwingine katika mazungumzo ya kitamthilia. Hivyo, tunajaribu kujibu maswali kama: Je, mazungumzo yanatokeaje kuwa ya kiunyanyasaji? Ni vipengele gani vya lugha vinadhihirisha unyanyasaji katika muktadha mahususi? Je, ni nini kinachomchochea mhusika amnyanyase mwenzake katika mahusiano ya kutongozana? Mhusika aliyenyanyasika huitikiaje?

## 2.0 Nadharia ya Uchanganuzi Tunduizi Kilongo wa Kifeministi

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Tunduizi Kilongo wa Kifeministi (kuanzia sasa, UTUKIKI) kama ilivyoasisiwa na kuelezwa na Lazar

(2005; 2007). Nadharia hii ilitokana na nadharia nyingine, Uchanganuzi Tunduizi Kilongo, ambayo inashughulikia dhima ya kilongo katika ujenzi na uendelezaji wa mamlaka katika jamii. Nadharia ya UTUKIKI ilisaidia katika kupanua Nadharia ya Uchanganuzi Tunduizi Kilongo kwa kuzingatia kikamilifu mambo ya ufeministi. Kwa hivyo, Nadharia ya UTUKIKI inathibitisha mchango wa ujinsia katika uhusiano wa kimamlaka, kama inavyodhihirika katika miktadha na jumuiya mbalimbali.

Tofauti na mikabala mingine ya kifeministi, UTUKIKI inalenga kuleta ukombozi unaozingatia haki na usawa kwa wote – wanawake na wanaume – kwa sababu wote ni binadamu (Lazar, 2007). Nadharia hii inabainisha umuhimu wa uhakiki katika ukombozi wa tabaka la chini, la wanyonge. Uhakiki katika nadharia hii unaangalia namna kilongo kinavyoendeleza mfumo dume katika jamii huku ukilenga kuleta mabadiliko chanya katika jamii, hususani uzingativu wa haki na usawa kwa mwanamke na mwanamume, kwa pamoja.

Aidha, UTUKIKI inaangalia ujinsia kama muundo wa kiitikadi ambao haujitokezi wazi kutokana na hali ya kwamba umefichika katika matumizi ya lugha na mikakati ya kilongo. Hii ni kwa sababu mamlaka ya kijinsia inaendelezwa kisiri, kupitia mila na desturi za kijamii ambazo zinazingatiwa na kutekelezwa katika mitagusano ya kimaongezi na kimaandishi. Hata hivyo, kwa mujibu wa Baxter (2008), nadharia hii – kwa namna ya kipekee – inachunguza kilongo kwa kuhusisha vipengele vingine, mbali na jinsia. Vipengele hivi ni kama ukabila, utabaka wa kiuchumi, umri, na viwango vya elimu ambavyo pia vinamuathiri binadamu kwa njia moja au nyingine.

Kwa jumla, UTUKIKI inasaidia katika kuthibitisha namna mamlaka inavyojitokeza na inavyoendelezwa katika matini husika. Shughuli hii inatekelezwa kwa kuchunguza matamko, vitendo, hadhi, majukumu na mienendo ya washiriki katika kitendo cha kijamii. Aidha, upinzani dhidi ya ubaguzi na ukatili wa kimamlaka unajitokeza na kuhimizwa kwa kutumia lugha faafu ambayo inadhihirisha usawa wa kijinsia. Nadharia ya UTUKIKI, kimsingi, inaangalia fasihi na/au uhakiki kama chombo cha kuleta mabadiliko faafu ya kijinsia katika jamii. Mabadiliko haya yanaweza kujitokeza katika ngazi ya mtagusano baina ya watu binafsi, na katika mahusiano ya kitaasisi katika jamii mahususi.

Katika makala hii, Nadharia ya UTUKIKI imesaidia katika kufafanua usawiri wa unyanyasaji wa kiusemi baina ya kijana wa kike Cheja na wa kiume Juma katika tamthilia ya *Hatia*. Kwa jumla, tumechunguza mtagusano wao ili kuelewa namna mazungumzo yao yanavyodhihirisha unyanyasaji wa kiusemi katika muktadha wa kimamlaka.

## 3.0 Muhtasari wa Tamthilia ya *Hatia*

*Hatia* ndiyo tamthilia ya kwanza kuchapishwa[1] na Penina Muhando ambaye, kwa mujibu wa Gibbe (1993) na Mwita (2009), ni mmojawapo wa waandishi maarufu wa tamthilia/fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania na katika eneo lote la Afrika Mashariki. Kulingana na Gibbe (*keshatajwa*), tamthilia ya *Hatia* iliigizwa kwa mara ya kwanza mwaka 1970 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na baadaye ikachapishwa mwaka 1972. Penina Muhando, ambaye pia hujulikana kwa jina lake la kindoa, Mlama (Zubkova na wenzake, 2009), ameandika tamthilia nyingine ambazo ni: *Tambueni Haki Zetu* (1973), *Heshima Yangu* (1974), *Pambo* (1975), *Harakati za Ukombozi*[2] (1982), *Nguzo Mama* (1982) na *Lina Ubani* (1984). Mbali na kutunga tamthilia na kuandika makala kadhaa za kihakiki, Mwita (2009) anaeleza kwamba umaarufu wa Muhando umetokana na kipawa chake katika kusawiri taswira angavu zinazodhihirisha matatizo ya jamii. Kwa msingi huo, makala hii imechukulia suala la unyanyasaji katika mahusiano ya vijana wanaotongozana kama mojawapo ya matatizo ya kijamii yanayodhihirishwa na mwandishi huyu.

Tamthilia ya *Hatia* inasawiri matatizo yanayomkabili Cheja, msichana mshamba aliyeenda kufanya kazi katika mazingira mapya ya kimji. Katika mazingira hayo yaliyo tofauti sana na mazingira ya malezi yake, Cheja analaghaiwa na kijana mwingine, Juma Bakari, mpenzi wake ambaye anampa ujauzito na baadaye kukana wajibu huo. Kwa 'kushauriwa' na Juma, Cheja anarudi nyumbani kwao akidai kuwa bosi wake, Bwana Sembuli ndiye alimpa ujauzito. Uongo huo unazusha mvutano mkubwa baina ya ukoo wa Cheja na wa Bwana Sembuli ambapo bosi huyo analaumiwa huku wazee wakidhani kwamba kweli ndiye mwenye hatia (Zubkova na wenzake, *keshatajwa*). Mwishowe, akieleza kwamba "Niliogopa kumtaja" mhusika (uk. 37), Cheja anatubu makosa yake na kuamua kuwa mkweli, asimfanye Bwana Sembuli kuumizwa bure. Hali hii inampa changamoto kubwa Cheja mpaka akafikiria kujinyonga. Cheja, hatimaye, anajitokeza kama mshindi anapowajibikia vitendo vyake na kuamua kwenda "kwenye kijiji kipya akajitegemee" (uk. 39) kwa kutafuta riziki na kumlea mtoto wake kwa heshima kama wazazi wengine. Mtazamo wa mwandishi ambao pia ni funzo kwa msomaji unadhihirishwa wazi katika maneno ya Cheja, akiomba msamaha kwa yote yaliyotokea, "Nimeshatambua kuwa maisha hayakimbiwi. Nisamehe!" (uk. 38).

Gibbe (1993) anaeleza kwamba *Hatia* iliwavutia watazamaji, wasomaji na wahakiki wengi kuliko tamthilia yoyote nyingine ya Muhando kwa sababu ya umwafaka wa maudhui, pamoja na uzuri wa mtindo wake. Tamthilia hii pia

---

[1] Kwa mujibu wa Zubkova na wenzake (2009), ingawa tamthilia ya *Hatia* ilichapishwa kabla ya tamthilia zake zote nyingine, tamthilia ya *Heshima Yangu* ambayo ilichapishwa mnamo mwaka 1974 ndiyo iliyoandikwa kwanza, mwaka 1968.

[2] Muhando aliandika tamthilia hii pamoja na waandishi wengine wawili: Ndyanao Balisidya na Amandina Lihamba.

imetungwa kwa lugha fasaha na yenye mnato, mtiririko mwepesi, pamoja na taharuki kubwa (Mugo, 1976). Vilevile, namna mwandishi alivyomfinyanga mhusika mkuu, Cheja – mvumilivu na mwenye ari, pamoja na kumpa ushindi baada ya matatizo mengi kuanzia pale aliposalitiwa na Juma – inaridhisha sana kwa msomaji. Gibbe (*keshatajwa*) anaeleza kwamba pamoja na kutazamwa na marehemu Rais wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, mnamo tarehe 5 Novemba 1970, tamthilia hii iliwapendeza na kuwavutia Watanzania wengi wakati wote ilipowasilishwa jukwaani.

Kuhusu suala la unyanyasaji baina ya vijana wanaotongozana, mahusiano kati ya Cheja na Juma yanashadidia wazi matatizo ya unyanyasaji huo katika jamii, na athari zake hasa kwa anayenyanyaswa. Cheja, "msichana [mbichi] mwenye umri wa miaka 17" (uk. 6) ambaye amewasili hivi majuzi mjini Dar es Salaam, anaanza mahusiano ya kimapenzi na Juma, "mvulana wa mjini mwenye umri wa miaka 20" (uk. 6). Hivyo, Juma anampa ujauzito Cheja na kwa bahati mbaya, anakana kuwajibikia ujauzito huo, jambo ambalo linamuumiza sana Cheja. Anapojitokeza kwa mara ya kwanza jukwaani, Cheja anaonekana mwenye wasiwasi, amekanganyikiwa, na "ana mawazo mengi na hatazami anakoelekea…," (uk. 7). Hali yake inaelezwa vizuri na Mvuvi aliyekutana naye hapo njiani:

Mvuvi: Eee! Mama wewe! Hatari kujiendea ovyo tu. Kama mambo yenyewe ndiyo kwenda tu bila kutazama walahi utajikuta uko dunia ya pili (uk.7).

Kwa hiyo, unyanyasaji wa Juma kwa Cheja kimsingi unahusisha mazungumzo juu ya ujauzito huo, na baadaye anavyoamua kumkana na kusitisha mahusiano yao. Maneno, vitendo na tabia ya Juma kwa jumla, vinamwacha mashakani Cheja, kama inavyodhihirika katika majibizano yao.

## 4.0 Kilongo cha Unyanyasaji wa Kiusemi katika Mazungumzo Baina ya Cheja na Juma

Unyanyasaji wa kiusemi unarejelea maneno, tabia na vitendo mahususi katika mtagusano wa kimaongezi ambavyo vinamfanya msemeshwaji ahisi hofu, uchungu, wasiwasi au kutojiamini ili mnyanyasaji/msemaji aweze kudhibiti hisi, mawazo na tabia za msemeshwaji huyo. Aidha, Dijk (1997) anaeleza kilongo kama taaluma inayofafanua matumizi ya lugha kwa kuzingatia jinsi lugha inavyotumiwa, kwa nini lugha hiyo inatumiwa na muktadha ambamo lugha hiyo inatumiwa. Kilongo kawaida kinathibitisha utabaka na kinalenga kuendeleza matakwa ya mamlaka fulani (Mulokozi, 2017). Garcia (1995) anasisitiza kwamba uchambuzi mwafaka wa kilongo katika matini ya kitamthilia unafaa kuhusisha maelekezo ya jukwaa, uzungumzi nafsi, na dayalojia yenyewe. Kwa hivyo, uchambuzi wetu wa kilongo cha unyanyasaji wa kiusemi baina ya Cheja na Juma katika tamthilia ya *Hatia* umezingatia vipengele hivyohivyo, ambapo tumezingatia tabia na mienendo

ya wahusika hao, maneno yao na wanavyoyasema, pamoja na jinsi wanavyojibizana.

Katika tamthilia hii, punde tu kabla ya Juma kujitokeza jukwaani, Cheja anatoa hisi zake katika uzungumzi nafsi ambapo anadhihirisha uchungu na majuto yake juu ya mahusiano yao, akisisitiza kwamba hapendi tena kuishi: "Wakati umefika ambapo sitamani tena kuishi, kuna faida gani kuishi ikiwa yote nipatayo ni uchungu na kupasukwa na moyo…" (uk. 7). Cheja hasa anazidi kuudhika akifikiria namna Juma alivyomlaghai kwamba anampenda ilhali kutaja "mapenzi" (uk. 8) kulikuwa kisingizio cha utashi wa kufanya ngono naye. Hatimaye, Cheja anajuta na kujilaumu, "Alinidanganya tu mwishowe akanikana. Nilifanya kosa kumwamini kijana kama yeye" (uk. 38). Kwa hivyo, "udanganyifu wa kimji" (Muhando, 1972[3]) au "ulaghai mtupu" (uk. 9), kama anavyotambua baadaye Cheja, ni kiini maalumu cha mamlaka wanayotumia vijana wa kiume wanaoishi mjini ili kuwatawala na kuwaumiza vijana wa kike ambao hawajazoea hali na mazingira ya kimji.

Kulingana na Herman (1998), jambo la msingi zaidi katika uchambuzi wa mazungumzo ya kitamthilia ni namna washiriki wanavyotekeleza zamu katika maongezi. Mtaalamu huyu anaeleza zamu ya maongezi kama haki au fursa anayopewa mshiriki ili aweze kushiriki vilivyo katika tukio au hali ya mtagusano wa kimaongezi. Hata hivyo, mshiriki mwenye mamlaka au hadhi kubwa anaweza kuingilia zamu ya mshiriki mnyonge (Bennison, 1998; Herman, 1998). Aidha, kwa kuzingatia utaratibu wa kimaongezi kinadharia, jozi za maongezi ya washiriki zinazokaribiana au kufuatana zinatarajiwa kujibizana au kuitikiana vilivyo kimuktadha (Goodwin & Heritage, 1990). Kwa kutomakinikia taratibu hizi, mshiriki mwenye mamlaka anamuudhi mwenzake asiye na mamlaka na hivyo kumfanya anyanyasike. Kwa mfano, Juma anaposalimiwa na Cheja, anatupilia mbali ukarimu huo kwa kutojibizana inavyotarajiwa:

Cheja: … Vipi?
Juma: (*Anahamaki*). Vipi nini? (uk. 8)

Hivi, Juma anaghadhabika badala ya kuitikia salamu za Cheja. Kitamaduni na kistaarabu, kutoitikia salamu ni tabia mbaya inayothibitisha upuuzi wa hali ya juu. Kupuuzwa na kutojaliwa kwa namna hii kunamuumiza na kumkera sana Cheja. Isitoshe, anayemfanyia maovu hayo ni mtu aliyemchukulia kuwa mpenzi wake, kama anavyoitikia kwa mshangao, "Haa, Juma mpenzi wangu. Ni wewe kweli…?" (uk. 8). Tamko la "Haa" hapa ni kama kilio kinachothibitisha maumivu aliyohisi Cheja, kutokana na mwitiko hasi wa Juma. Kadhalika, neno "mpenzi" limetumiwa tu kukejeli unafiki wa Juma kwani tabia yake haidhihirishi upendo tena. Kwa jumla, tabia na maneno ya Juma yamedhihirisha hasira ambayo ni mojawapo ya kategoria za unyanyasaji wa kiusemi (Evans, 2006). Juma ametumia hasira kama

[3] Ufafanuzi wa mwandishi unaopatikana kwenye jalada la nje la tamthilia ya *Hatia*.

mkakati wa kuendeleza mamlaka yake, huku akimtisha, akimkanganya na kumdhibiti Cheja. Katika hali hii, Juma amejitokeza kifahari na kumfedhehesha vikali kijana wa kike ambaye anaonekana mnyonge.

Cheja pia anastaajabika na kuumizwa kutokana na jinsi Juma anavyofungua maongezi yake bila ya ukarimu au hisi za upendo. Juma ameshangaa tu kumuona tena Cheja lakini kamwe hadhihirishi furaha, kama mtu ambaye amekutana na mpenzi wake. Anathibitisha wazi kwamba hana haja tena na Cheja, kulingana na maswali anayomuuliza: "Unafanya nini…? Unatoka wapi na unakwenda wapi?" (uk. 8). Hali hii inampa wasiwasi na uchungu Cheja, na ndiyo sababu anaamua kumjibu ovyo kwamba anaenda "Popote" (uk. 8). Mwitiko wa Cheja unathibitisha kwamba amekatishwa tamaa na msimamo wa Juma kuhusu mahusiano yao.

Halikadhalika, Cheja anapotangaza, "Nina jambo la kukwambia…" (uk. 8), Juma anamkatisha kauli kwa "kumkodolea macho" (uk. 8) na hivyo kumtisha akiuliza, "Jambo gani?" (uk. 8). Vitisho ni namna nyingine inayotumiwa na mwenye mamlaka kumnyanyasa kiusemi na vilevile, kumdhibiti mnyonge. Aidha, baada ya kumuudhi hivi Cheja, Juma angetarajiwa kufanya tendo la kiungwana kwa kujaribu kuomba msamaha kama njia ya kurejesha uhusiano mwema katika mazungumzo yao. Ingawa mara nyingi havijitokezi au kutambulika kwa uwazi, vitendo na tabia za aina hii hasa vinapofanywa na 'mpenzi' vinaumiza kihisia na ni jambo ambalo linampa wasiwasi na kumfanya anyanyasike zaidi Cheja. Kinadharia, unyanyasaji wa aina hii una misingi yake katika itikadi ya kijinsia ambayo, kwa malezo ya Lazar (2007), inalenga kudumisha utabaka ambao unaendeleza mfumo dume katika jamii.

Katika jitihada za kuepukana na ukatili na unyanyasaji wa Juma, Cheja anaamua kunyenyekea na kuzungumza "polepole" (uk. 8) huku akimwambia, "Nina mimba" (uk. 8). Kinyume na matarajio ya Cheja, Juma anamfokea zaidi anaposikia hivyo. Wingi wa hasira na ukali unamfanya Juma atumie sentensi fupifupi huku akiuliza, "Una mimba?" "Yangu mimi?" (uk. 8). Halafu ananyamaza ghafla na kujifanya kusahau au "kama hakusikia kitu" (uk. 8). Ukimya, kujifanya kusahau, na kukana ukweli ni tabia za kiunyanyasaji ambazo huwa zinalenga kumwingiza wasiwasi, kumkanganya, na pengine kumfanya ajilaumu mwenyewe msemeshwaji. Aidha, hali hiyo humfanya maskini aliyenyanyasika kutoelewa la kuongezea. Hivyo, katika mkanganyiko huo, Cheja anaona afadhali abadili mada kidogo akisema, "Sasa tupange la kufanya" (uk. 8). Hapo Juma anaamua kumuumiza zaidi huku akipinga kabisa maoni ya Cheja, na kukariri kwa msisitizo: "Haya panga basi, panga" (uk. 8). Kisha, Juma anajifanya tena kama hakusikia vizuri maombi ya Cheja ya "tupange," anapouliza, "Unasema tupange na nani?" (uk. 8) na kusisitiza, "Yanakuhusu wewe mwenyewe" (uk. 8). Lawama kali za namna hii zinamgandamiza sana Cheja huku pia akiwa ametengwa na kuachwa mpweke. Ajabu ni kwamba mnyanyasaji hubaki katili vile, habadiliki. Hata Cheja anaponyenyekea huku akisema kwa upole, Juma bado anaitikia kwa ukali akilenga

kumuumiza maradufu Cheja. Hii inathibitisha vile mwenye mamlaka hupenda kumdhibiti wakati wote mnyonge ili kuimarisha utawala wake zaidi.

Aidha, usaliti wa Juma ambapo anamtendea kinyama Cheja ilhali akimrejelea kimzaha kama “dada,” ni kitendo cha kikatili zaidi. Unyanyasaji wa kimzaha unaumiza maradufu kwani unamgandamiza huku pia ukimkanganya kimawazo msemeshwaji. Bila kuamini maneno ya kinafiki ya “mpenzi” wake, Cheja anamuuliza, “Umesema nini, Juma?” (uk. 8). Badala ya kuitikia moja kwa moja, Juma anamjibu kwa upuuzi akiuliza, “Wewe umesikia nini?” (uk. 8) halafu anamfokea “kwa ukali” (uk. 8) akidai, “…unanicheleweshа sina wakati mimi” (uk. 8). Baada ya kumtia wasiwasi na uchungu vya kutosha, Juma anaanza hapohapo kuondoka ili kumuumiza zaidi. Tofauti za hali na hadhi ya kila mmoja wao zinadhihirika kupitia usambamba wa maneno wanayotumia. Huku Cheja akimwona Juma kuwa ‘mpenzi’ wake, Juma anamrejelea tu kama ‘dada.’ Namna hiyo, lugha ya Juma inamtenga na kumuudhi Cheja, huku akitambua ukweli kwamba anachukiwa kuliko kupendwa.

Kwa kuzidiwa na uchungu, Cheja pia anaamua kujitetea “kwa hamaki” (uk. 8) kama binadamu wa kike anayekariri malalamiko na maumivu yake kwa mwenzake wa kiume: “Huwezi kunikana… unataka kunikana hivi. Hata kidogo!” (uk. 8). Hapo Juma anaitika kimzaha akisema, “Hata kikubwa” (uk. 8). Usambamba huu, yaani ‘hata kidogo’ na ‘hata kikubwa’ unadhihirisha hadhi au tabaka zao tofauti. Juma anajitokeza kama mwenye kiburi huku Cheja akionekana kama mnyonge asiye na uwezo wa kujitetea kikamilifu. Hata anapojaribu kujitetea, Juma anamwapia huku akimtisha zaidi kwamba asipotenda kama anavyoamriwa, “Walahi utajuta” (uk. 8).

Aidha, Juma anajiona fahari na mwenye mamlaka zaidi, huku akimdhalilisha Cheja. Hii ndiyo maana Juma anaitika kwa kicheko cha dharau na kejeli. Juma pia anamuuliza Cheja maswali machungu yanayomchoma kama sindano huku akimkumbusha kwamba yeye (Juma) ni mvulana wa mjini Dar es Salaam, asiyetishika: “Utafanya nini... utaniona wapi? Dalisalama hii, dada, utanikuta wapi? Kwanza nani shahidi?” (uk. 8). Ukatili huu unamfanya Cheja kuzungumza “kwa uchungu” (uk. 9) usio kifani, hususani baada ya kugundua kwamba Juma hana haja na mtoto atakayezaliwa: “Hunifikirii nitamfanyaje mtoto” (uk. 9). Fikira hii inamuumiza Cheja mpaka ashindwe cha kusema “kwa muda” (uk. 9).

Isitoshe, Juma anajitokeza kama binadamu asiye na huruma kulingana na namna anavyomkata kauli na kumpinga moja kwa moja Cheja. Juma anatumia usambamba tena ili kumdhihirishia wazi Cheja, nani kati yao ni mwenye nguvu na nani mnyonge:

Cheja: Siamini! Siamini!
Juma: Amini! Amini tu! (uk. 9)

Badala ya kushauriana kwa pamoja juu ya kushughulikia ujauzito na namna ya kumlea mtoto wao, Juma anamtaka tu Cheja aondoke mbele zake, arudi tu kwa wazazi wake, "Jiendee zako kwa wazazi wako ukajitunze…" (uk. 9). Juma hamjali na hamhurumii Cheja, na ndiyo sababu anajitenga naye na kumtolea kauli ya ovyo na ya kupotosha, "Nende tu" (uk. 9). Anapomuuliza atawaambieje wazazi wake, Juma kimakusudi anapuuza hoja hiyo kwa "uovu" (uk. 9), eti Cheja awaambie kwamba anayehusika na ujauzito ni mwajiri wake, Bwana Sembuli. Juma anamlaghai kwamba maelezo hayo pia wazazi wake Cheja "wataamini tu" (uk. 9). Kuyachukulia kwa urahisi hivi mambo ambayo kwa kweli ni mazito sana ni kitendo cha kusikitisha ambacho bila shaka kinamuumiza vikali Cheja. Upuuzi na upotoshaji huo unamshitua na kumkera sana Cheja mpaka ashindwe "kuvumilia kusikia zaidi" (uk. 9) isipokuwa kuzidiwa na huzuni na hivyo, kuangua kilio, "Uuuuuuui! Sitaki kusikia zaidi, Uuuuuuuuuuui!" (uk. 9). Kuona kwamba amefikia kilele cha unyanyasaji na udhibiti wake ambapo amemliza Cheja, Juma "anakimbia" (uk. 9) bila kumliwaza au hata kumwambia 'Pole!' Hata hivyo, Juma haondoki bila kumchoma Cheja kwa vitisho zaidi: "…usije akathubutu kunitaja… utapata taabu" (uk. 9). Kweli maneno, tabia na vitendo vya Juma vimemfanya maskini Cheja anyanyasike kiasi kwamba hajielewi na hawezi kujitetea zaidi.

Aidha, kama alivyoingia jukwaani na kuanza mtagusano na Cheja bila salamu, Juma anamwacha 'mpenzi' wake bila 'kwaheri.' Kitendo hiki ambacho ni cha kimaksudi kinathibitisha upotofu wa maadili na pia kinakiuka utaratibu wa kimaongezi. Hiyo ni tabia ya kinyama inayoonesha ukatili na inamfanya Cheja anyanyasike kimawazo na kiakili.

Kadhalika, ukatili umedhihirika katika maelekezo ya jukwaa ambapo mwandishi anafafanua maudhui yake kwa kueleza nini wahusika wanachotenda, namna wanavyotenda, na mienendo au tabia zao (Garcia, 1995). Hivyo, uchambuzi wa maelekezo ya jukwaa umechangia sana katika kuangaza na kuthibitisha zaidi unyanyasaji wa kiusemi katika mazungumzo baina ya Cheja na Juma. Mifano kadhaa ya maelekezo ya jukwaa inamdhihirisha wazi Juma anavyomnyanyasa kiusemi kijana mwenzake katika mahusiano, kama ifuatavyo:

Juma: (*Anahamaki*) (uk. 8) – kugadhabika/hasira ni upuuzi na pia njia ya kumtisha Cheja.

Juma: (*Akimkodolea macho*) (uk. 8) – kutumbua macho ni kitendo cha kumtisha mhusika.

Juma: (*Ananyamaza kama hakusikia…*) (uk. 8) – anajifanya hivi ili kumkanganya Cheja.

Juma: (*Kwa ukali*) (uk. 8) – anamfokea na kumuamuru kifahari ili kumtisha Cheja.

Juma: (*Anacheka*) (uk. 8) – ni kicheko cha dharau ili Cheja ajihisi hana hadhi yoyote.

Juma: (*Anaondoka haraka*) (uk. 9) – baada ya kumuumiza ili ahisi upweke na uchungu.

Katika mifano hii, Juma anajitokeza kama mhusika bapa ambaye ni katili, mlaghai, na mwenye kiburi. Juma wakati wote analenga kumpuuza, kumgandamiza na kumdhibiti Cheja, huku mwenyewe akijikinga dhidi ya hatia yoyote na vile kuendeleza hadhi na mamlaka yake. Kwa upande mwingine, maelekezo ya jukwaa yanayomhusu Cheja yanadhihirisha namna anavyofedheheshwa na kunyanyasika. Hali na hadhi yake inathibitisha unyonge, uchungu na mkanganyiko wa kimawazo na kiakili:

> Cheja (*polepole*) (uk. 8) – Amenyanyasika na kunyenyekea; Juma amemtisha na kumdhibiti.
> Cheja (*kwa hamaki*) (uk. 8) – Ameamua kujitetea lakini Juma anamuapia kuwa atajuta.
> Cheja (*kwa uchungu*) (uk. 9) – Ni uthibitisho wa kunyanyasika kwa unyonge.
> Cheja (*Anashindwa kusema kwa muda*) (uk. 9) – Amenyanyasika hadi kukata tamaa.
> Cheja (*Anashutuka*) (uk. 9) – Maneno ya Juma yamemchoma; haamini anayoyasikia.
> Cheja (*Anashindwa kuvumilia kusikia zaidi*) (uk. 9) – Ameumizwa, avunjika moyo; alia.

Kwa hivyo, katika uchambuzi wa mtagusano wa kimazungumzo, maneno ya washiriki yanategemeana na tabia na vitendo vyao, pamoja na maelekezo ya jukwaa katika kutimiza dhamira ya mwandishi, na kusawiri maudhui mahususi. Aidha, uchambuzi huo umesaidia katika kufafanua lugha na muktadha wa kimamlaka kama vipengele mahususi vya kilongo cha unyanyasaji wa kiusemi baina ya Cheja na Juma kama vijana katika mahusiano ya kutongozana.

## 5.0 Hitimisho

Suala la unyanyasaji wa kiusemi baina ya vijana katika mahusiano ya kutongozana linadhihirika katika tamthilia ya *Hatia*. Juma, anasawiriwa kama katili ambaye anamlaghai kimapenzi Cheja katika mahusiano yao. Vijana kama Juma hawako tayari kuwajibikia wenzao katika mahusiano hayo na ndiyo maana baada ya kumpa ujauzito, bila ya hisi za kiutu, Juma anamkana kabisa Cheja, na hata hajali mtoto wao atakayezaliwa atakuzwaje. Kwa kutumia Nadharia ya UTUKIKI, makala hii imefafanua kilongo cha unyanyasaji wa kiusemi baina ya vijana wanaotongozana. Kilongo cha unyanyasaji huo kinajikita katika matumizi ya lugha hasi na muundo wa kimajibizano unaothibitisha utabaka baina ya wahusika. Juma ambaye ni kijana wa kiume amejitokeza kama mwenye mamlaka ambapo anatumia mamlaka hiyo kumdhalilisha na kumnyanyasa Cheja, kijana wa kike ambaye anaonekana mnyonge.

Unyanyasaji wa kiusemi hasa umedhihirika kupitia vitisho na ukali, kukana na kumpinga wazi msemeshwaji na hoja zake, kumpuuza kwa kutumia lugha ya

kimzaha, kejeli na kicheko cha dharau, kughadhibika, lawama na kukata kauli, na kumnyamazia au kumjibu visivyo msemeshwaji. Kulingana na mfano wa Cheja, unyanyasaji wa kiusemi kwa jumla unakanganya, unaleta uchungu, hofu na maumivu makali kwa mnyonge anayenyanyaswa. Aidha, kwa kuzingatia Nadharia ya UTUKIKI, tunaona kwamba mamlaka ya kijinsia ambayo inajikita katika mfumo dume yanachangia sana katika uendelezaji wa unyanyasaji wa kiusemi baina ya vijana wanaotongozana. Cheja amenyanyasika vikali hasa kwa sababu ni kijana wa kike. Juma ni kijana wa kiume ambaye ni sehemu ya tabaka la juu, yaani la wenye mamlaka, ilhali Cheja anawakilisha tabaka la chini; tabaka la wanyonge wasio na uwezo katika mienendo ya kijamii. Inaonekana ni kama Juma anamthibitishia Cheja kwamba 'hata ukifanya juu chini, wewe mwanamke mnyonge huwezi kujinasua, huwezi kunitisha, isipokuwa tu kuendelea kuumia.'

Halikadhalika, Juma anatumia ufahari wake kama kijana mwenye uzoefu wa mazingira ya mjini kumdanganya Cheja. Kama msichana mshamba, Cheja hayaelewi mazingira ya mjini na ndiyo maana analaghaiwa kwa urahisi. Hoja hii inaungwa mkono na maelezo ya mwandishi kwenye jalada la tamthilia hii anaposema, "*Hatia* ni mchezo unaotuonyesha matatizo yanayotukabili tunapoishi kwenye mazingira yenye misingi tofauti na ile tuliyolelewa nayo." Kwa msingi huo, unyanyasaji wa Juma dhidi ya Cheja unaweza kuhusishwa na ufahari wa Juma kama mwenye uzoefu wa mazingira hasi ya kimji.

Aidha, kuna uwezekano kwamba Juma anamkanganya na kumdhibiti Cheja kwa sababu anamzidi umri. Juma ni kijana mwenye umri wa miaka ishirini huku Cheja akiwa na miaka kumi na saba. Labda wangekuwa na umri sawa, Cheja angetambua mapema tabia za Juma na ulaghai wake na hivyo kujihadhari au kumkimbia kabla ya kumpa ujauzito. Kwa jumla, mnyonge Cheja amethibitisha sifa na tabia nzuri na vilevile anaibuka kama mshindi mwishoni mwa tamthilia. UTUKIKI inapendekeza uhakiki kama njia ya kukomboa tabaka la chini. Ushindi wa Cheja unaashiria ukombozi wake. Kwa namna hii, wema na uwajibikaji umefaulu ilhali Juma ameshindwa kwa ukatili na maovu yake.

## Marejeleo


Apsler, J. and Duggan, E. (2012). Teen Dating Violence, *Domestic Violence Services Network*, www.loveisrespect.org, accessed on 22 August, 2018.

Baxter, J. A. (2008). "Feminist Post-structurist Discourse Analysis – A New Theoretical and Methodological Approach?" In Harrington, K., Litosseliti, L., Sautson, H., Sunderland, J. (Eds). *Gender and Language Research Methodologies*, 13: 243-255.

Bennison, N. (1998). "Accessing Character Through Conversation – Tom Stoppard's Professional Foul." In Culperer, J., Short, M. & Verdonk, P. (Eds.). *Exploring the Language of Drama: From Text to Context*. London: Routledge. pp. 67-82

Herman, V. (1998). "Turn Management in Drama," In Culperer, J., Short, M. & Verdonk, P. (Eds.). *Exploring the Language of Drama: From Text to Context*. London: Routledge. pp. 19-33.

Evans, P. (2006). *The Verbally Abusive Man: Can He Change?* Massachusetts: Adams Media.

Garcia, J. (1995). Some Reflections on the Analysis of Discourse and Dramatic Text: Stoppard's *Jumpers*, *Revista Alicantina de Estudios Ingleses*, 8: 161-167.

Gibbe, A. G. (1993). "Women and the Making of Swahili Literature in East Africa," A Report of the Project that was Sponsored by OSSREA.

Goodwin, C. & Heritage, J. (1990). Conversational Analysis, *Annual Review of Anthropology*, 19:283-307.

Hagan, J. na Foster, H. (2001). Youth Violence and the End of Adolescence, *American Sociological Review*, 66(6): 874-899.

Lazar, M. M. (2005). "Politicizing Gender in Discourse: Feminist Critical Discourse Analysis as Political Perspective and Praxis," In M. M. Lazar (Ed.). *Feminist Critical Discourse Analysis*. London: Blackwell. Pp. 1-28.

Lazar, M. M. (2007). Feminist Critical Discourse Analysis: Articulating a Feminist Discourse Praxis, *Critical Discourse Analysis Studies*, 4 (2): 141-164.

Leaver, M. (2002). "Adolescent Dating Violence and Identity Development: A South African Perspective," MA Thesis, Stellenbosch University.

Lethbridge, S., and Mildorf, J. (2004). *Basics of English Studies: An Introductory Course for Students of Literary Studies in English*. Stuttgart and Freiburg: Universities of Tubingen.

Lewis, S. F. and Fremouw, W. (2001). Dating Violence: A Critical Review of the Literature, *Clinical Psychology Review*, 21(1):105-127.

Mugo, M. G. (1976). Geroshon Ngugi, Peninah Muhando and Ebrahim Hussein: Plays in Swahili, *African Literature Today*, 8:137-141.

Muhando, P. (1972). *Hatia*. Nairobi: East African Publishing House.

_______(1973). *Tambueni Haki Zetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

_______ (1974). *Heshima Yangu*. Nairobi: East African Publishing House.

_______ (1982). *Pambo*. Dar es Salaam: Swala Publications.

_______ (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press

_______ (1984). *Lina Ubani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Muhando, P., Balisidya, N. na Lihamba, A. (1982). *Harakati za Ukombozi*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mwita, B. M. (2009). Uhakiki wa Mtindo na Maudhui katika baadhi ya Tamthilia za Penina Mlama, *Mulika*, 28:104-128,

Oliveira, R.N.G., Gessner, R., Brancaglioni, B.C.A., Fonseca, R.M.G.S. & Egry, E.Y. (2016).

Preventing Violence by Intimate Partners in Adolescence: An Integrative Review, *Journal of School of Nursing*, 50 (1):134-143.

PCADV (2011). *Pennsylvania Coalition Against Domestic Violence – Teen Dating Violence*. www.pcadv.org, accessed on 20 August, 2018.

Rubio-Garay, F., Lopez-Gonzalez, M.A., Carrasco, M.A, and Amor, P.J. (2017). The Prevalence of Dating Violence: A Systematic Review, *Psychology Papers*, 38 (2): 135-147.

Salari, S. M. and Balwin, B. M. (2002). Verbal, Physical, and Injurious Aggression among Intimate Couples Over Time, *Journal of Family Issues*, 23 (40): 523-550.

Swart, L., Seedar, M., Stevens, G. and Ricardo, I. (2002). Violence in Adolescents' Romantic Relationships: Findings from a Survey Amongst School-going Youth in South African Community, *Journal of Adolescence*, 25 (4):385-395.

WHO (1989). World Health Organisation Report on the Health of Youth, https://apps.who.int>WHA42_TD-2_eng, accessed on 21 December, 2019.

Wood, K. and Jewkes, R. (2001). "Violence, Rape and Sexual Coercion: Everyday Love in South African Towship," In Whitehead, S. and Barrett, F. (Eds.). *The Masculinities Reader*, 133-140. Cambridge: Polity Press.

Wubs, A.G., Aaro, L.E, Flisher, A.J., Bastien, S., Onya, H.S., Kaaye, S. and Mathews, C. (2009). Dating Violence among School Students in Tanzania and South Africa: Prevalence and Socio-demographic Variations, *Scandinavian Journal of Public Health*, 37 (2):75-86.

Zubkova, E.B., Gromov, M. D., Khamis, S. A. M., and Wamitila, K. W. (2009). *Outline of Swahili Literature: Prose Fiction and Drama* (2nd Edition). Boston: Brill.